

MATUMAINI PROG NO:2525

TITLE: WHOM DO MEN SAY THAT I AM ?

SUMMERY: KINAZUNGUMZIA KUYAHUSU MAONI YA WATU KUMHUSU KRISTO .

TEXT: MATHAYO 16:13-20

MADA: WATU HUSEMA MIMI NI NANI?

.....

U hali gani msikilzaji wangu popote ulipo nikiwa nakukaribisha kwenye kipindi hiki cha leo. Ni tumaini langu ya kuwa unaendelea vizuri kupitia kwa upendo wake Mwenyezi Mungu. Mimi nami kwa upande wangu niko swadakta kabisa nikimshukuru Mungu.

Hebu kwanza kabisa tukapate kuomba kabla ya kusonga mbele.

Natuombe;

OMBI....Mwanzilishi wa vyote na tena Baba yetu uliye Mbunguni ,,tunakuja tena mbele zako na ombi la kutaka usaidizi wako wa kiroho ili tukaweze kulielewa fundisho hili la leo. Asante kwa sababu nafasi hii.

Ni kwa Yesu tumeomba Amen

Ni wakati mwinguine tunapopatana tena angani ili kufundishana nawe kulihusu neno lake Mwenyezi Mungu.

Hiki ni kipindi cha Matumaini kutoka TWR Kenya.

Mada au ukipenda ujumbe wetu wa leo ni,,, *watu husema mimi ni nani?* Somo ni kutoka kwenye Injili ya Mathayo 16:13-20.

Kwa kulimalizia fundisho hili la leo,,,bila shaka,,,nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano ili tukaweze kusidiana kwa pamoja.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa njia kama hii,,,.....

WIMBO:

Ni Producer JT Raf,,akifanya cover ya wimbo Usinidharau Leo

ulioimbwa na mtutumishi Israel Mbonyi.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Rafiki yangu,,, kwa karne nyingi, wanatheolojia, wachungaji, wasomi na hata wanafalsafa wamekuwa wakitafakari kwa kina kuhusu vile ambavyo Bwana wetu Yesu Kristo anapotambuliwa. Wengine, bila ya kujua,,wamehoji kama aliwahi kuishi kabisa,,, wakipendekeza kuwa Injili zilizoandikwa ni kazi za waandishi wa hadithi za kubuni na si rekodi halisi za kihistoria.

Wengine husema huenda wakati fulani kulikuwa na mhubiri tu aliyesafiri sehemu mbalimbali za Palestina na kuvutia fikra za watu wa kawaida,,, lakini kuamini kuwa alikuwa na asili ya kimungu ni jambo gumu sana kwao kulikubali.

Mpendwa,,, ukweli ni kwamba hata Alexander Mkuu au ukipenda kwa kiingereza Alexander the great, miaka 300 kabla ya Kristo, hakujua kikamilifu matokeo yote ya ushindi wake,,, lakini alitumiwa na Mungu kuutayarisha ulimwengu kupitia kwa njia ya utawala.., lugha ya Kigiriki, na amani ya muda kwa ajili ya kuja kwa Kristo na kuenea kwa Injili.

Mpendwa, mwandishi Eric Sauer katika kitabu chake *The Dawn of World Redemption* anasema kwamba mabadiliko makubwa yaliyotokea duniani pamoja na kushuka kwa maadili,, yaliandaa watu kuupokea ujumbe wa Mungu. Hii inaonyesha kwamba wakati ambao Mungu alikuwa ameupanga ulikuwa umefika.Naam, Bwana na asifiwe sana!

Sasa, katika Injili ya Mathayo 16:13-20,,, tunapata kisa hiki cha kuisisimua ambacho Biblia inatuambia ya kwamba;

13. Yesu alipofika pande za Kaisaria-Filipi, aliwauliza wanafunzi wake, akisema, "Watu husema mimi, Mwana wa Adamu, ni nani?"

14. Nao wakasema, "Wengine husema wewe ni Yohana Mbatizaji; wengine Eliya; na wengine Yeremia, au mmojawapo wa manabii."

15. Akawaambia, "Nanyi mnasema mimi ni nani?"

16. Simoni Petro akajibu akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

17. Yesu akajibu akamwambia, "Heri wewe, Simoni Bar-Yona; kwa maana mwili na damu havikufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni."

18. Nami nakuambia, "Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."

19. Nami nitakupa funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.

20. Kisha akawaonya wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye ndiye Yesu Kristo.

Rafiki yangu, kutokana na fungu hili la Biblia, tunaona majibu matatu makuu yanayotusaidia kumjua Yesu Kristo ni nani.

Katika kulichambua neno hili,,tunapata kukiona Kipengele cha kwanza kabisa kikiwa ni,,, Maoni ya Kawaida ya Umma.

Katika aya ya 14,,, wanafunzi walitoa majibu yaliyohusishwa na matukio ya hivi karibuni au mapokeo ya kale.

Kuna wale waliosema ya kuwa,,,Yesu ni Yohana Mbatizaji,,,kama Mfalme Herode aliyesumbuliwa na dhamiri ya kwamba ,,,,Yohana aliyemkata kichwa alikuwa amefufuka tena.

Wengine walisema ni Eliya, yule nabii mkuu wa Mlima Karmeli,,, na wengine Yereimia au mmojawapo wa manabii.

Vivyo hivyo leo rafiki yangu,,, maoni ya watu wengi hata wa leo yanakosa kumtambua Kristo pamoja na lengo lake halisi.

Wanamwona tu kama mwalimu mkuu wa maadili kwa sababu ya Mahubiri ya Mlimani,,, wengine mwanamapinduzi aliyetetea maskini,,, au mtumishi mkuu wa Mungu.

Lakini nakuambia,,, mitazamo hii ya kibinadamu inakosa lengo halisi!

Kipengele cha pili ndugu yangu,,,ni kinahusiana na,,, Jibu la Kibinafsi. Yesu hakutaka tu kuyajua maoni ya umma; alitaka ungamo la mioyo yao. Ndio maana katika aya ya 15 aliuliza: "*Nanyi mnasema mimi ni nani?*" Na hapo ndipo Petro aliposimama na kutoa lile jibu zito na la kipekee: "*Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.*"

Ndugu yangu,,, neno "Kristo" linatokana na lugha ya Kigiriki *Christos*,,, likimaanisha "Aliyepakwa Mafuta" au Masihi. Huyu ndiye yule ambaye Isaya alitabiri habari zake na Yesu akazisoma katika Luka 4 kwamba ametia mafuta kuwahubiria maskini habari njema. Kusema "Mwana wa Mungu aliye hai" lilikuwa tamko nzito sana kwa Myahudi anayeamini Mungu ni mmoja,,, lakini Petro alitambua Utatu na Uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo!

Kiwango cha tatu na cha mwisho kwa leo kutokana na fungu hili,,, ni kuhusiana na,,, *Ufunuo Wenye Kusudi Maalum*. Katika aya ya 17,,, Yesu anamwambia Petro: "*Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.*"

Dadangu,,, ubinadamu peke yake hauna uwezo wa kufahamu siri hii kuu. Ilihitaika mawasiliano ya moja kwa moja kutoka mbinguni!

Kamas Eric Sauer alivyofafanua katika kitabu chake, *The Triumph of the Crucified*,,, kuingia kwa Kristo katika mwili ndio kitovu cha mabadiliko ya nyakati zote na kilele cha juu cha upendo.

Na juu ya mwamba huu wa ufunuo na ungamo la Petro,,, ndipo Yesu alipoahidi kulijenga kanisa lake, akitoa na mamlaka ya funguo za ufalme zinazodhibitiwa na mbingu. Hii ni dhana ya udhibiti wa kiungu,,, na neno la mbingu ndilo neno letu!

Kwa kumalizia msikilizaji wangu,,, nataka tukakumbushane kwa muhtasari viwango hivi 3 vya mtazamo kuhusu utambulisho wa Yesu Kristo ili nasi tukaingie katika ukweli kamili:

Kwanza kabisa, ni kuepuka maoni ya juu-juu ya umma yanayomwona Yesu kama mwalimu au mwanafalsafa tu.

Pili, ni kuwa na jibu na ungamo la kibinafsi la kumtambua Yeye kama Kristo na Masihi aliyepakwa mafuta kwa ajili yetu.

Tatu na mwisho, ni kupokea ufunuo wa kiungu kutoka kwa Baba, ambao ndio msingi imara kama mwamba wa kanisa na maisha yetu.

Kukiri kwamba Yesu ndiye Kristo,,, ni kutoka katika giza la ulimwengu huu na kuingia katika nuru tukufu ya Injili.

Ningependa kukuacha na neno hili la Kutia Moyo kutoka kwenye 1 Petro 2:9 linalosema:

"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."

Amina!

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili kuhusiana na *vile ambavyo Mwanao Yesu Kristo anavyo tambulika*.Kwa kweli nasi tunamtambua kama Kristo Bwana wetu.Tutumie Roho wako wako ili akatusaidie katika kuishikilia imani hii .
Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni swali la Bwana wetu Yesu Kristo kwa wanafunzi wake kwamba,,,Je! *watu husema mimi ni nani?*

Tumeutoa kwenye Mathayo 16:13-20

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo nakutazama wewe tu naye Christopher Mwahangila ...

WIMBO.....

Asante sana Mtumishi Chistopher Mwahangila kwa kazi hiyo nzuri ya kubariki

kweli kweli,,.....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505
NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke
Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri